

GREDI YA 3
MTIHANI WA MWISHO WA
MUHULA WA KWANZA 2023
KISWAHILI SEHEMU YA A

1. Ufahamu
2. Sarufi
3. Kuandika
4. Kusikiliza na Kuzungumza

Jina _____

Shule _____

Gredi _____

Jinsia

Mvulana _____ Msichana _____

KWA MATUMIZI YA MTAHINI

Tumia vigezo na viwango vya kuthaminia vilivyopewa kwenye mwongozo wa mwalimu.

	Kuzidisha Matarajio	Kufikisha Matarajio	Kukaribia Matarajio	Mbali Na Matarajio
Kusikiliza na kuzungumza	9-10	7-8	6-5	0-4
Kusoma kwa sauti	68	60	50	40-20
Ufahamu	9-10	8-7	5-6	0-4
Sarufi	13-15	10-12	5-9	0-4

ZOEZI LA KWANZA: UFAHAMU

Soma hadithi kisha ujibu maswali.

Shule yangu inaitwa shule ya msingi ya Bidii. Shule hii ina wanafunzi wengi. Mimi niko katika gredi ya tatu. Darasa letu lina wanafunzi thelathini. Rafiki yangu ni mzuri na anawapenda wanafunzi. Shule yetu ina bustani ndogo. Katika bustani hii, kuna miti mingi.

a) Shule hii inaitwaje?

b) Shule hii ina wanafunzi wangapi?

c) Mwalimu wao anaitwa nani?

Yusuf aliamka akiwa na furaha. Mjomba wake alikuwa amewapangia ziara. Ilikuwa ziara ya kutembelea mbuga ya wanyama ya Masai Mara. Bwana Fadhili, mjomba wake alikuwa amekodi gari la kuwapeleka ziara hiyo.

a) Kwa nini Yusuf aliamka akiwa na furaha?

b) Ni nani alikuwa amewapangia ziara?

c) Andika wanyama wawili waliowaona.

Yerula anaishi kijiji cha Baraka. Yeye ana bibi na binti mmoja. Bibi yake anaitwa Asha. Asha ni mkulima hodari. Yerula ni mwalimu katika shule ya msingi ya Maji Mazuri. Yeye anapenda kazi yake.

a) Je, Yerula anaishi wapi?

b) Ni nani mwalimu kati ya Asha na Yerula?

c) Bibi yake Yerula ni nani?

d) Asha ni _____ hodari.

ZOEZI LA PILI: MATUMIZI YA LUGHA

I. Andika vizuri majina haya.

a) iilmb _____

b) eembj _____

2. Kamilisha sentensi hizi.

a) Mbegu hupandwa kwenye _____ (udongo, nyasi)

b) Wiki moja ina siku _____

3. Unda maneno ukitumia silabi

a) mw _____

b) pw _____

c) nd _____

4. Andika sentensi hizi kwa kutumia maneno haya.

a) Mzalendo

b) Bendera

c) Shujaa

5. Chora na utaje vifaa viwili vya shambani..

6. Ambatanisha neno na maana yake kwa kuchora mstari.

nadhifu	sababu ndogo ndogo
kuomba radhi	chooni
msalani	safi
visingizio	kuomba msamaha

7. Chagua jibu sahihi.

a) _____ hufanya kazi ya ukulima.

b) _____ hulinda lango la shule.

c) Daktari hutibu _____

8. Andika kwa maneno.

a) 7I _____

b) 22 _____

9. Jaza nafasi kwa herufi inayofaa.

Da _ ati

10. Tumia 'yeye' au 'wao' kujaza mapengo.

_____ anaruka kamba

II. Chagua jibu sahihi kujaza nafasi

Jane a ___ fagia darasa kesho asubuhi. (na, li, ta)

ZOEZI LA TATU: KUANDIKA

Binadamu anaweza kuishi vizuri akiwa na _____ (nguo,

usalama) wa kutosha. Usicheze na vitu _____ (hatari,

furaha) kama vile _____ (moto, chombo). Usimwamini kila

_____ (mtu, kitu) ambaye humjui. Ukiona hali ya hatari,

usinyamaze pig _____ (magoti, kelele). Watu watakuja

kusaidiana.

ZOEZI LA NNE: KUSTKILIZA NA KUZUNGUMZA

Mwalimu atakusomea hadithi hii kisha atakuuliza maswali.

Hawa ni sungura wawili. Sugura mmoja ni mweupe na wa pili ni mweusi.

Sungura mweupe ni mfupi. Sungura mweusi ni mrefu.

a) Je, sungura ni wangapi?

b) Sungura mmoja ni _____

c) Sungura mwingine ni _____

- d) Ni sungura yupi mfupi?
- e) Sungura mweusi ni_____
- f) Sungura wangapi wametajwa kwenye hadithi _____
- g) Wingi wa sungura ni_____
- h) Hadithi hii ni kuhusu nini? _____
- i) Rangi zipi zimetajwa kwa hadithi?

KUSOMA KWA SAUTI (maneno 70 kwa dakika moja)

Mim ninaitwa Tume. Nina umri wa miaka saba. Rafiki yangu anaitwa Busara. Tunasoma katika shule moja. Busara ana umri wa miaka saba kama mimi. Siku yake ya kuzaliwa ni tofauti na yangu.

Mimi ninapenda kusoma hadithi. Busara anapenda kuimba nyimbo. Wakati mwingine hutunga wimbo mfupi. Sisi huimba pamoja. Mimi pia hutunga hadithi. Nina penda hadithi za wanyama wadogo.

Mimi na Busara tunapenda mchezo wa mpira. Busara anaupenda mchezo huu zaidi. Busara hunifurahisha sana. Yeye anapenda kutazama mchezo wa mpira kwenye runinga. Mchezaji akifunga bao yeye hurukaruka.

Wakati mwingine Busara hunishangaza. Yeye hata anaweza kulia mchezaji akishindwa. Mimi humuuliza kwa nini analia. Yeye huniambia hapendi watu wawe na huzuni. Hakika Busara ni rafiki wangu wa kweli.